

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI



Simu:2555-732980745

Fax: 255-732980745

Baruapepe: ded@misungwidc.go.tz

Tovuti:www.misungwidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
Kitengo cha Teknolojia,Habari,

Mawasiliano na Uhusiano

S.L.P 20

MISUNGWI.

TAARIFA KWA UMMA

**KUKANUSHA HABARI YA MILLIONI 82 KUTAFUNWA MISUNGWI ILIYOANDIKWA
KATIKA GAZETI LA UHURU LA TAREHE 8 JANUARI 2018.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Eliurd Mwaiteleke anapenda kuwataarifu Wananchi wote na Umma kwa ujumla kwa kukanusha taarifa ya Habari yenye Kichwa cha Habari "Millioni 82 zatafunwa Misungwi"na Mtendaji akimbia na Mashine ya EFD iliyochapishwa na kutolewa katika Gazeti la Uhuru la Jumatatu tarehe 8 Januari 2018 kwenye Ukurasa wa kwanza na Ukurasa wa tatu iliyoeleza kwamba Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango ya Halmashauri imehakiki vyanzo vya Mapato na kubaini "Madudu"ya Wizi wa fedha uliosababishwa na baadhi ya Watendaji wa Kata na Idara ya Mapato .

Habari hiyo ilieleza na kuthibitisha kwamba fedha hizo Millioni 82 zimetafunwa na Mchwa wa Halmashauri na kusababisha kushuka kwa Mapato ya mwezi Novemba 2017 kutoka Tsh,Millioni 170 hadi Tsh,Millioni 88 wakati huo huo Mtendaji wa Kijiji cha Mwawile akikimbia na Mashine ya Kielektroniki ya kukusanyia Mapato pamoja na Kitabu cha kumbukumbu za makusanyo ya Ushuru wa Mazao ya kizuizi cha Mwawile.

Hivyo, kutokana na taarifa na Takwimu halisi zilizopo za Makusanyo ya Mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi hususani kwenye chanzo cha Mapato ya Ushuru wa Mazao kilichopo katika Kizuizi cha Mwawile Kata ya Nhundulu ambacho katika Mfumo wa Mapato unaonyesha tangu Agosti 2016 hadi Januari 8, 2018 zimekusanywa jumla ya Tsh, 19,054,000 ambao ni Ushuru wa Mazao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi anautaarifu umma kuwa taarifa iliyochapishwa si ya kweli na yenye nia na lengo la kupotosha umma kuhusu shughuli za Ukusanyaji wa Mapato ambazo zinafanywa na Watendaji wa Kata na Vijiji kwa kutumia

Mashine za Kielektroniki za kukusanyia Mapato (POS) kutokana na sababu na mambo yafuatayo:-

i/. Taarifa za Mapato zilizopo hazionyeshi upotevu na Wizi wa Tsh,Millioni 82 kama ilivyochapishwa katika Gazeti la Uhuru la tarehe 8 Januari, 2018.

ii. Taarifa ya Ukaguzi na Uhakiki wa vyanzo vya Mapato uliofanywa na Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango kuanzia tarehe 3 hadi 5, Januari 2018 haijatolewa na kuwasilishwa kwenye kikao cha Kisheria kilichoagiza cha tarehe 27 Disemba, 2018.

iii. Mwandishi wa Habari hiyo hakufanya Mahojiano na Msemaji wa Halmashauri (Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya) kuhusiana na Wizi unaodaiwa,kwa mujibu wa Mienendo na Maadili ya Uandishi wa Habari yanavyobainisha ili kuthibitisha ukweli .

iv. Ifahamike kwamba Mtendaji wa Kijiji cha Mwawile Ndugu, Felician Mhala hakutoweka na Mashine ya Kukusanyia mapato (POS) na vitabu vya makusanyo isipokuwa hakuwepo katika eneo la kazi kwa siku husika na tayari ameshafika ofisi ya Mapato kuhakiki Mashine hiyo pamoja na kuwasilisha takwimu za makusanyo.

Natoa Rai na kuwakumbusha Waandishi wa Habari na Watanzania wote kuendelea kutumia uhuru wa kupata na kutoa habari kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo na tunazidi kuwaomba kufanya mawasiliano na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kwa ajili ya kupata taarifa na habari mbalimbali kuhusu shughuli na Miradi ya Maendeleo zenye ukweli na usahihi kwa kuongeza uwazi na uwajibikaji na kuleta maendeleo kwa Watanzania.

2

“Misungwi tupo tayari kukuhudumia kwa Maendeleo yako”

“MWANZA: KAZI NA MAENDELEO”

“ KAZI NA MAENDELEO: MWANZA”

Imetolewa na:



Thomas Lutego

Kaimu:Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini (W)

MISUNGWI

8 Januari, 2018